ISSN 2820-2686 | Toleo No. 10 | Januari - Machi | 2024

# JARIDA LA WAKILI MKUU





## Mafanikio ya Miaka Mitatu ya MHE. SSH katika OWMS

ICC INTERNATIONAL CHAMBER OF COMMERCE



**DKT. SAMIA SULUHU HASSAN**
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

# BODI YA UHARIRI

## Mwenyekiti

**Mark Eldad Mulwambo**

Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali

## Mhariri Mkuu

**Prisca Jackson Ulomi**

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

## Waandishi wa Jarida

**Prisca Jackson Ulomi**

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**Dennis Julius Buyekwa**

Afisa Habari

## Msanifu wa Jarida

**Nyamhoni Robert Chacha**

Afisa TEHAMA

## Wajumbe

**Salome Samuel Magesa**

Kaimu Mkurugenzi wa usuluhishi

**Hangi Matekeleza Chang'a**

Mkurugenzi Msaidizi Katiba, Haki za Binadamu na Uchaguzi

**Kiuye Mbwana Shemakame**

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Maktaba na Utafiti

**CPA Devota Mathew Ngulugulu**

Mhasibu Mkuu

**Mercy Rowland Kyamba**

Mkurugenzi Msaidizi - Udhibiti Ubora

**Zuhura Mohamed Kussaga**

Mchumi

# TAHARIRI

Toleo la Kumi la Jarida la Wakili Mkuu ni maalumu kwa ajili ya kuangazia mafanikio ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) katika kipindi kinachoanzia mwezi Januari, 2024 mpaka Machi, 2024 kwa kuzingatia 4R za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inatambua umuhimu wa kuendeleza falsafa ya 4R zilizoasisiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Rais Samia Suluhu Hassan ambazo ni Maridhiano (Reconciliation), Mabadiliko (Reform), ujenzi mpya (Rebuild) na ustahimilivu (Resilience) kwa kuzingatia maadili haya muhimu yameiwezesha OWMS kuboresha utendaji wake.

Kwa kutambua umuhimu wa 4R, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imefanikiwa kuokoa fedha nyingi baada ya kuanza kutumia njia ya Maridhiano (Reconciliation) katika kuendesha mashauri yake kwa njia ya usuluhishi hatua ambayo imeisaidia Serikali kutumia fedha zilizookolewa katika kuboresha huduma za wananchi kama vile ujenzi wa vituo vya afya nchi nzima, barabara, na miradi ya kimkakati ya ujenzi wa Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere na Reli ya Kisasa (SGR).

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inaamini katika kuendesha mashauri kwa njia ya majadiliano kwa kuwa njia hii imesaidia kuongeza mahusiano bora kati ya Serikali na wawekezaji hatua ambayo imesaidia kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini kama ambavyo Mhe. Rais Dkt. Samia anaamini maridhiano na maelewano yanawezekana kwa kukaa pamoja na kujadiliana kwa njia ya mazungumzo na hivyo kuleta tija katika kulileta Taifa maendeleo.

Aidha, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imekuwa ikiamini katika kuendesha mashauri kwa weledi hasa katika kuongoza majadiliano kwa kuzingatia ustahimilivu ambao umesaidia Ofisi kuendesha majadiliano hayo kwa kuvumiliana na upande wa pili wawekezaji hasa katika kuainisha changamoto na jinsi ya kukabiliana nazo ili kuzitafutia ufumbuzi wa kudumu ili Serikali iweze kupunguza idadi ya mashauri yanayoweza kufunguliwa dhidi yake.

Kwa kuzingatia muktadha wa 4R, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inatambua kuwa Mabadiliko (Reforms) hayaepukiki katika ujenzi wa nchi kwani kuleta maendeleo endelevu kunahusisha mageuzi na kwa dhana hiyo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kuboresha na kutumia mifumo ya TEHAMA katika uendeshaji wa mashauri yake ambapo sasa Mawakili wa Serikali wanaendesha mashauri na majadiliano kwa njia ya mtandao kwa mashauri ya ndani na nje ya nchi hatua ambayo imeongeza ufanisi wa uendeshaji wa mashauri hayo.

Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imeweka msukumo mkubwa katika kuleta mageuzi makubwa katika kila nyanja ikiwemo mageuzi ya sera, sheria na kanuni mbalimbali ili kuakisi mazingira ya wakati tulionao katika kuwavutia wawekezaji na hivyo kufikia azma ya kupiga hatua kimaendeleo.

Kuhusu kutekeleza dhana ya kujenga upya (Rebuiding), Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imekuwa inashirikiana vyema, kushauri na kusimamia vyema uingiaji wa mikataba ambavyo imekuwa moja ya msisitizo mkubwa wa Mhe. Rais Dkt. Samia katika ujenzi wa nchi kwa kutambua kuwa kazi kubwa za maendeleo zimefanyika katika awamu zote tano za watangulizi wake.

Kwa kwa kutambua umuhimu wa 4R na mchango wake katika kuiletea nchi yetu maendeleo, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali itaendelea kufanya kazi kwa weledi kuhakikisha kwamba 4R ambazo ni Maridhiano (Reconcilation), Ustahimilivu (Resiliency), Mabadiliko (Reform) na Kujenga Upya (Rebuilding) zinaendelea kutekelezwa kwa vitendo.

Toleo hili kwa upekee lina makala mbalimbali za kitaaluma zinazotokana na majukumu mama ya Ofisi yenye lengo la kutoa elimu kuhusu maamuzi mbalimbali pamoja mahusiano ya Ofisi na taasisi nyingine. Mwisho, Toleo hili linaangazia namna ambavyo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilimuaga na kuomboleza kifo ndugu Solomoni Lwenge aliyekuwa Wakili wa Serikali Mfawidhi mkoa wa Shinyanga.

Mambo haya na mengine mengi yataakisiwa ndani ya Jarida hili. Naomba nimalizie kwa kuomba wasomaji wetu kuendelea kutoa maoni kwa Bodi ya Uhariri kwa ajili ya kuboresha Jarida hili ili kwa pamoja tuweze kulifanya Jarida hili kutoa mchango chanya katika ukuaji wa Sekta ya Sheria hapa nchini. Nawatakia usomaji mwema wa Toleo la Kumi la Jarida la Wakili Mkuu. Asanteni.



Prisca Jackson Ulomi
**Mhariri Mkuu**

# Kutoka Kwenye Dawati la Mwenyekiti wa Bodi ya Uhariri

Toleo la Kumi la Jarida la Wakili Mkuu ni maalumu kwa ajili ya kuendelea kuangazia mafanikio ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) katika miaka mitatu ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kuangazia hilo, Jarida hili linaendelea kutambua mchango mkubwa wa Rais, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika maeneo ya bajeti, ujenzi wa Ofisi kwenye mji wa Serikali, Mtumba jijini Dodoma, usimamizi wa mashauri, mifumo ya usimamizi wa mashauri na udhibiti ubora, mafunzo kwa watumishi wa OWMS, ushirikiano wa Ofisi na wadau, maboresho ya mifumo ya TEHAMA ambayo kwa kiasi kikubwa yameboresha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ndani na nje ya nchi.


Pamoja na mafanikio haya yanayotokana na mchango mkubwa wa Mhe. Rais Dkt. Samia, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imekuwa mstari wa mbele katika kuhimiza na kusisitiza mambo mbalimbali yanayohusu OWMS na nchi kwa ujumla na nafasi ya watumishi katika kutunza uadilifu na siri za Serikali.

Toleo hili pia kwa sehemu kubwa linaangazia ushiriki wa OWMS katika Maadhimisho ya kilele cha Wiki ya Sheria, ushiriki wa OWMS kwenye mkutano Mkuu wa Chama cha Mawakili wa Serikali (PBA) pamoja na nafasi ya Ofisi katika kutatua migogoro kwa njia ya usuluhishi ikiwa ni kuziishi falsafa za 4R zilizoasisiwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sambamba na hayo, Toleo hili linaangazia nafasi ya OWMS katika kutoa msaada wa kisheria wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika Jijini Dodoma, pamoja na namna ambavyo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imekuwa ikitumia 4R za Mhe. Rais Dkt. Samia kwa kushughulikia migogoro ya usuluhishi inayofunguliwa dhidi ya Serikali.

Aidha, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali itaendelea kuwa mdau mkubwa katika kukuza uchumi wa Taifa katika utekelezaji wa majukumu yake ambayo ni kuiwakilisha Serikali na taasisi zake katika Mahakama na mabaraza ndani na nje ya nchi. Toleo hili pia litagusia namna OWMS imeokoa fedha za Serikali kupitia mashauri fedha ambazo zingelipwa kwa walalamikaji iwapo Serikali ingeshindwa kesi Mahakamani. Matukio yote haya ni sehemu ya utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na wadau wake.

Naomba nimalizie kwa kuwaomba wasomaji wetu kuendelea kutoa maoni kwa Bodi ya Uhariri kwa ajili ya maboresho ya Jarida hili ili kwa pamoja tuweze kulifanya Jarida hili kutoa mchango chanya katika ukuaji wa Sekta ya Sheria hapa nchini pamoja na kuboresha utendaji na ufanisi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Nawatakia usomaji mwema wa Toleo la Kumi la Jarida la Wakili Mkuu. Asanteni





Mark Eldad Mulwambo
**Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali**

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| UK. 06 | Rais Samia Atoa Wito wa Kuimarisha Mfumo wa Haki Madai |
| UK. 10 | Mafanikio ya miaka mitatu ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali |
| UK. 14 | Waziri wa Katiba na Sheria asisitiza Mawakili wa Serikali kuwa Waadilifu Wanapotekeleza Majukumu Yao |
| UK. 17 | Migogoro Dhidi ya Serikali Katika Mikataba ya Kimataifa: Nini Kifanyike Ili Wizara na Taasisi Zake Kuepuka Migogoro |
| UK. 21 | 4R Katika Kushughulikia Migogoro ya Usuluhishi Dhidi ya Serikali |
| UK. 24 | OWMS Yamaliza Mashauri Yenye Maslahi Mapana kwa Taifa |
| UK. 28 | Habari Picha |
| UK. 31 | OWMS Yajiandaa Kupokea Mashauri Ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa |
| UK. 35 | OWMS Kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Mashauri wa Mahakama Kuu |
| UK. 37 | Serikali Mbioni Kuanzisha Kituo cha kushughulikia Kero za Wananchi |
| UK. 39 | Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu Watakiwa Kufahamu Sheria za Vyuo Vyao |
| UK. 41 | Serikali Yashinda Shauri la Usuluhishi Katika Baraza la Kimataifa la Biashara (ICC) |
| UK. 43 | PEPMIS kuongeza uwajibikaji kwa Watumishi wa Umma |
| UK. 45 | TANZIA |




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza na Viongozi pamoja na wageni mbalimbali walioshiriki Maadhimisho ya Kilele cha Wiki ya Sheria nchini ambayo Kitaifa yamefanyika katika viwanja vya Chinangali Jijini Dodoma tarehe 01 Februari, 2024.*

# Rais Samia Atoa Wito wa Kuimarisha Mfumo wa Haki Madai

Idadi ya Majaji wa Mahakama ya Rufani imeongezeka kutoka Majaji 16 mwaka 2021 hadi Majaji 35 hili ni sawa na ongezeko la 118%, wakati Majaji wa Mahakama Kuu wameongezeka kutoka 63 mwaka 2021 hadi 105 mwaka 2023 ongezeko la 67%,

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amewaongoza watanzania kuadhimisha Siku ya Sheria na kutoa wito kwa wadau wa Haki Jinai nchini kutumia njia ya usuluhisi zaidi katika kutatua migogoro ili kuweza kuimarisha Haki jinai nchini.

Rais Samia aliyasema hayo wakati wa Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Sheria nchini yaliyofanyika katika Viwanja vya Chinangali Jijini Dodoma.

Akizungumza wakati wa Maadhimisho hayo Mhe. Rais Samia alisema kuwa upo umuhimu wa kuimarisha pia mfumo wa haki madai kwa kuwa bado mfumo huo una matatizo katika uendeshaji wa mashauri, ambapo kesi zinacheleweshwa kwa kuwa na mzunguko mrefu na kupelekea shauri moja kutumia hadi miezi 12 katika Mahakama zetu za Wilaya na Mahakama ya Hakimu Mkazi kuanzia zinaposikilizwa hadi kuhitimishwa.

Kuhusu uendeshaji wa mashauri kwa upande wa Mahakama Kuu Mhe. Rais Samia alisema kuwa uendeshaji wa kesi umekuwa ukichukua mpaka miezi 24 kwa shauri moja linapoanza kusikilizwa hadi kutolewa hukumu, ambapo alisema kuwa ili kuepuka kutumia muda mrefu katika kuendesha mashauri, matumizi ya njia ya usuluhishi yatatusaidia katika kuongeza ufanisi kwa kupunguza muda wa kuendesha mashauri haya na haki kupatikana kwa wakati.

Aliongeza kuwa ni vyema kutumia njia ya usuluhishi katika kushughulikia mashauri haya kwa kuwa njia ya usuluhishi tofauti na Mahakama hauachi makovu ya hasira hivyo kutoa nafasi ya wadaawa kufanya kazi pamoja bila kuhitilafiana hivyo usuluhishi unaweza kuwa ni njia nyingine ya kuimarisha haki madai.

Mhe. Rais Samia ameendelea kusisitiza kuhusu kuharakishwa kusikilizwa kwa kesi za kibiashara, kwa kufafanua kuwa upo uhusiano mkubwa kati ya haki na maendeleo ya kiuchumi, mwekezaji anathamini sana muda kwani muda ni mali, mitazamo ya wadau wa Mahakama ijielekeze kwenye kupunguza muda unaotumika kwenye uendeshaji wa mashauri.

Kuhusu kuanzishwa kwa Kampeni ya Msaada wa kisheria ya Mama Samia Mhe. Rais Samia amefafanua kuwa Kampeni hiyo ilianzishwa kwa sababu yalikuwepo malalamiko mengi kwa wananchi ya kupata msaada wa kisheria. Tangu kuanzishwa kwa kampeni hiyo imewafikia wananchi 383,293 katika mikoa 6 na kufanikiwa kutatua jumla ya migogoro 511.

Aliahidi kuwa Serikali itaendelea kuimarisha utendaji kazi wa Mahakama kwa ujenzi wa Mahakama za kisasa ikiwemo kuongeza Mahakama za Vituo Jumuishi nchi nzima pamoja na kuongeza idadi ya wafanyakazi kila bajeti itakaporuhusu.

Akitoa mfano kuhusu namna alivyoboresha muhimili wa Mahakama nchini, Mhe. Rais amesema kuwa idadi ya majaji wa Mahakama ya Rufani imeongezeka kutoka majaji 16 mwaka 2021 hadi majaji 35 hili ni sawa na ongezeko la 118%, wakati majaji wa Mahakama Kuu wameongezeka kutoka 63 mwaka 2021 hadi 105 mwaka 2023 ambalo ni ongezeko la 67%. Serikali inatazamia kuwa na uwekezaji mkubwa uliofanywa kwenye majengo na ongezeko la majaji utaongeza ufanisi wa Mahakama katika utoaji haki.

Kwa upande wake Jaji Mkuu wa Tanzania Mhe, Jaji Ibrahim Hamis Juma amemshukuru Mhe. Rais Samia kwa kutoa fedha za kujenga majengo ya Mahakama nchi nzima ikiwemo Vituo Jumuishi ambavyo kwa kiasi kikubwa vimesaidia kuimarisha utoaji haki nchini na kwa wakati.

Naye Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi akizungumza katika maadhimisho hayo alisema kuwa Serikali inakusudia kuwa na kituo cha huduma wezeshi kitakachotoa huduma masaa 24 kwa kila mkoa ili wananchi waweze kupata elimu ya msaada wa kisheria kuelewa taratibu na hatua za kuchukua pale wanapopata changamoto.

Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wameshiriki kilele cha maadhimisho hayo wakiongozwa na Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Ndg. Mark Mulwambo ambapo wakati wa maadhimisho hayo, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilitoa elimu ya msaada wa kisheria kupitia banda la maonesho namba 23 lilokuwa katika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma.


> "Serikali itaendelea kuimarisha utendaji kazi wa Mahakama kwa ujenzi wa Mahakama za kisasa ikiwemo kuongeza Mahakama za vituo jumuishi nchi nzima ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya Wafanyakazi kila bajeti itakaporuhusu,"




*Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Prof. Ibrahim Hamis Juma akizungumza na Viongozi pamoja na wageni mbalimbali walioshiriki Maadhimisho ya Kilele cha Wiki ya Sheria nchini ambayo Kitaifa yaliyofanyika katika viwanja vya Chinangali Jijini Dodoma.*




*Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi akizungumza na Viongozi pamoja na wageni mbalimbali walioshiriki Maadhimisho ya Kilele cha Wiki ya Sheria nchini ambayo Kitaifa yaliyofanyika katika viwanja vya Chinangali Jijini Dodoma.*



*Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakiwa kwenye viwanja vya Chinangali yanapofanyika Maadhimisho ya Kilele cha Wiki ya Sheria nchini, ambapo Mgeni Rasmi wa maadhimisho hayo alikuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.*




*Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Ndg. Mark Mulwambo (aliyesimama katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mara baada ya Maadhimisho ya Kilele cha Wiki ya Sheria yaliyofanyika katika Viwanja vya Chinangali Jijini Dodoma.*





# Mafanikio ya Miaka Mitatu ya MHE. SSH katika OWMS

INTERNATIONAL CHAMBER OF COMMERCE



**DKT. SAMIA SULUHU HASSAN**
**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilianzishwa tarehe 13 Februari, mwaka 2018 kupitia Hati Idhini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyotolewa kwa mujibu wa Ibara ya 36 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 50 la Mwaka 2018 ikiwa na majukumu ya kusimamia, kuratibu na kuendesha mashauri yote ya madai, usuluhisi, Katiba, haki za binadamu na uchaguzi.

Katika kipindi cha miaka mitatu (03) cha Uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan ambacho ni 19 Machi, 2021 hadi Februari 2024, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeiwakilisha Serikali na Taasisi zake kwa ufanisi na ubora katika mashauri yote ya madai na usuluhishi.

Katika kutekeleza jukumu hili, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeshughulikia mashauri ya madai yaliyoihusisha Serikali na Taasisi zake ambapo katika kipindi tajwa, Ofisi imefanikiwa kushughulikia jumla ya mashauri ya madai 5,111 na kushinda mashauri 2,165 ambapo Ofisi imefanikiwa kuokoa shilingi 1,291,671,108,713.47.

Kwa upande wa mashauri ya usuluhishi, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kipindi cha uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendesha jumla ya mashauri ya usuluhishi 153. Kati ya hayo, mashauri 139 ni ya usuluhishi wa kitaifa na mashauri 12 ni ya usuluhishi wa kimataifa. Aidha, hadi kufikia Februari 2024, mashauri 59 yalimalizika katika Mahakama, Mabaraza na kwa njia ya majadiliano. Baadhi ya mashauri ambayo Serikali imeshinda na yanahusisha fedha taslimu, Serikali imeokoa kiasi cha shilingi 6,757,788,034,101 na dola za Marekani 829,699,740.75.

Vilevile, katika kipindi cha miaka mitatu (03) ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeendelea kuratibu na kuendesha vikao vya majadiliano ya kumaliza migogoro nje ya Mahakama na Mabaraza. Hadi kufikia Februari 2024, jumla ya mashauri 13 ya usuluhishi wa Kimataifa na mashauri matano (05) ya usuluhishi wa Kitaifa yanaendelea katika majadiliano.

Katika kipindi cha miaka 3 ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imefanikiwa kuendesha mashauri mbalimbali kwa mafanikio makubwa, baadhi ya mashauri hayo ni kama ifuatavyo:-

i) Shauri la Kikatiba la Gideon Wasonga dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Rufaa Na. 37/2018 ambalo mnamo tarehe 23 Desemba 2021, Mahakama ilitoa ushindi kwa Serikali, hivyo kuiepusha Serikali kufanya mchakato wa kubadilisha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kwa kuondoa dhamana kwenye makosa makubwa ya jinai, kitu ambacho kingeleta madhara kwenye ustawi na umoja wa nchi;

ii) Shauri la Kikatiba la James Francis Mbatia dhidi ya Job Yustino Ndugai, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wenzake, maombi Na. 2/2022 ambalo mnamo tarehe 28 Januari, 2022, Mahakama ilitoa ushindi kwa Serikali, hivyo kuiepusha Serikali na gharama ya kurudia mchakato wa upatikanaji wa Spika na Naibu Spika na kuiondoa nchi katika taharuki ya mgogoro wa kikatiba ambao ungeweza kutokea kutokana na shauri hilo;

iii) Shauri la kikatiba la Onesmo Olengurumwa dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Maombi Na. 09/2021 ambalo tarehe 15/02/2022 Serikali ilishinda kwa Mahakama kukubaliana na hoja za Serikali kwamba mwananchi anapaswa kuthibitisha kwamba ameathirika na uvunjifu wa haki za binadamu kabla ya kudai haki hiyo mahakamani. Uamuzi huu utasaidia kupunguza mashauri yasiyo na msingi ya uvunjifu wa haki za binadamu dhidi ya Serikal;

iv) Shauri la kuzuia ujenzi wa bomba la Mafuta baina ya Center for Food and Adequate Living Rights na wenzake watatu dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Uganda na wenzake watatu lenye Maombi Na. 39/2020 lililomalizika tarehe 30/11/2023 katika Mahakama ya Afrika Mashariki ambapo kumalizika kwa shauri hilo kumesababisha ujenzi wa bomba hilo kuendelea kutekelezwa kama ilivyokuwa imepangwa;

v) Shauri la Madai ya Kazi la Shirika la Posta Tanzania dhidi ya Dominic Kilangi, Rufaa ya Madai Na. 12/2022 ambalo mnamo tarehe 26 Machi, 2022 Mahakama ya Rufaa ilitoa ushindi kwa Serikali na kutatua mkanganyiko wa kisheria uliokuwepo kwa muda mrefu kuhusiana na taratibu za kufuatwa baada ya

watumishi wa umma waliofanya kazi katika Taasisi za Serikali kuachishwa kazi. Uamuzi huu utasaidia kuhakikisha taratibu zilizowekwa na Serikali katika mashauri hayo zinafuatwa na hivyo kuepusha ukiukwaji wa sheria zilizotungwa na Serikali. Kadhalika, uamuzi huo unasaidia kupunguza msongamano wa mashauri ya kazi yanayohusu watumishi wa umma yaliyokuwa yakiendelea katika vyombo visivyo na mamlaka ya kuendesha mashauri hayo pamoja na gharama za kuendesha mashauri hayo. Kwa sasa mashauri ya kazi yamepungua hadi kufikia mashauri 185 mwezi Desemba 2023 ukilinganisha na mashauri ya kazi 375 yaliyokuwepo hadi kufikia Desemba 2021 kabla ya uamuzi huo;

vi) Kufungua mashauri mbalimbali yaliyoiwezesha Serikali kurejesha madeni ya wadaiwa sugu wa Serikali kwenye madai ya pango, umeme mfano mnamo tarehe 14 Juni, 2023 kupitia shauri la Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Bodi ya Pamba Tanzania dhidi ya We Africa Tanzania Limited, Shauri la Ardhi Na.50/2023, Serikali iliweza kurejesha kodi ya kiasi cha dola za Marekani 1,058,568 kutoka kwa wadaiwa sugu wa Bodi ya Pamba Tanzania;

vii) Pia, Ofisi imekuwa ikitoa utaalamu wa kisheria kwenye Kampuni na taasisi ambazo Serikali ina maslahi mathalani katika shauri la Mwanasheria Mkuu wa Serikali dhidi ya Mirage Lite Ltd & Airtel Tanzania Ltd, maombi ya madai Na. 647/01/2023 Serikali iliwezesha fedha kiasi cha shilingi 2,977,041,000 iliyokuwepo kwenye akaunti ya Benki ya Kampuni ya Airtel Tanzania isikamatwe na kumlipa mdai ambae hastahili fedha hizo. Pia, Serikali kwa kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliweza kushirikiana na Mawakili binafsi waliokuwa wakisimamia Rufaa ya benki ya CRDB dhidi ya Symbion Power (T) Limited, Rufaa ya Madai Na. 371/2022 na kuiwezesha benki ya CRDB kushinda Rufaa hiyo tarehe 5/9/2023 na kuokoa kiasi cha shilingi bilioni 34 kilichokuwa kinadaiwa na Symbion pasipo halali;

viii) Vilevile, Serikali kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilishirikiana na Mawakili binafsi waliokuwa wanasimamia Shauri la Airtel Tanzania Limited dhidi ya Ose Power Solution Limited, rufaa ya madai Na. 206/ 2027 na kuiwezesha Kampuni ya Airtel kushinda Rufaa hiyo tarehe 20 Desemba, 2021 na kuokoa kiasi cha shilingi 1,920,473,771.79 na dola za Marekani 143,484.72 kilichokuwa kinadaiwa na Kampuni ya Ose Power Solution isivyo halali; Aidha, tarehe 31 Oktoba 2023, Serikali ilishinda Shauri la Ose Power Solution Limited dhidi ya Airtel Tanzania Limited, maombi ya madai Na. 45/01 ya 2022 ambalo lilihusu maombi ya marejeo dhidi ya uamuzi wa Mahakama ya Rufani uliyoipa ushindi Kampuni ya Airtel kama ilivyoelezwa hapo juu;

ix) Tarehe 27 Oktoba, 2023 katika shauri la Chalinze Cement Company Limited na wenzake dhidi ya Tume ya Ushindani na wenzake, Maombi ya Baraza Na. 41/2023, Serikali ilifanikiwa kushinda shauri hili ambapo kwa kumalizika kwake imewezesha Kampuni ya Twiga na Tanga Cement kumalizika kuendelea na uwekezaji;

x) Mnamo tarehe 10 Agosti, 2023 na tarehe 02 Oktoba, 2023; Ofisi ilimaliza mashauri matatu (03) ya Kikatiba (Alphonce Lusako & 3 Others vs. The Attorney General & 3 Others, Misc. Civil Cause No. 5 of 2023, Meczedeck Maganya v. The Attorney General & 2 Others and Misc. Civil Cause No. 09 of 2023 Fredrick Antony Mboma Vs AG) yaliyokuwa yanapinga uwekezaji katika Bandari ya Tanzania na kusaidia kurudisha imani ya watu kwa Serikali na uwekezaji huo kuendelea; na

xi) Shauri la Paul Emanuel Kisabo dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, maombi ya madai Na. 9/2022 linalopinga muda wa Ofisi wa Jaji Mkuu ambapo kwa kumalizika kwa shauri hilo kumeisaidia Serikali kulinda Katiba na kuheshimu mamlaka ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mashauri mengine yaliyoendeshwa kwa mafanikio na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni kama yafuatavyo:-

i) Humphrey Simon Malenga dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Seriali, maombi ya madai Na. 07/2023 na Mpale Kaba Mpoki dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Prof. Ibrahim Hamis Juma, maombi ya madai Na. 11/2023 ya kupinga muda wa Ofisi wa Jaji Mkuu;

ii) Blue Pearl Hotel dhidi ya Ubungo Plaza na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, maombi ya madai Na. 103/2021 ambapo Serikali ilifanikiwa kupata hukumu ya madai ya kodi yadola za Marekani 2,702,507.95;

iii) M/S Simba Logistics Equipment Supply Ltd dhidi ya Mamlaka ya Rufani ya Manunuzi ya Umma na TAZARA, maombi

ya madai Na. 39 & 41 ya ununuzi wa vifaa vya reli;

iv) Halima James Mdee wenzake dhidi ya Bodi ya Wadhamini wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo na wenzake, maombi ya madai Na. 27/2022;

v) Tito Elias Magoti na wenzake dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, maombi ya madai Na. 3/2022 ya Sheria ya Uchaguzi;

vi) M/S Leighton Offshore Pte Ltd dhidi ya Mamlaka ya Bandari Tanzania, shauri la biashara Na. 114 la mwaka 2017 lenye madai ya uvunjifu wa mkataba wa dola za Marekani 12,064,628;

vii) Shauri la Uchaguzi la Sebastian Antony Mbilingwa dhidi ya Msimamizi Msaidizi wa Kata ya Mbabala, Mwansheria Mkuu wa Serikali na wenzake, shauri la rufaa la uchaguzi Na. 41/2022;

viii) Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (PSSSF) dhidi ya Kampuni ya Estim Construction Company Limited, shauri la maombi ya biashara Na. 16/2023;

ix) The Voi Sisal Estate Limited dhidi ya Katibu Mkuu, shauri la madai Na. 62/2015la (mgogoro wa ardhi lenye thamani ya paundi 48,032,000 sawa na shilingi bilioni 172;

x) Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji dhidi ya Overseas Infrastructure Alliances Pvt Limited, shauri la madai Na. 5/2020; na

xi) Cosmos Developers Ltd na Mwenzake dhidi ya Mark Auctioneers na Court Brokers Company Ltd, Azania Benki na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Shauri la Ardhi Na. 29/2020 kuhusu mgogoro wa ardhi Serikali ilishinda hukumu ya dola za Marekani 2,681,000 baada ya wadaiwa kukiri eneo la mgogoro ni mali ya Serikali.

Katika hatua nyingine Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imekuwa ikiendesha mashauri kwa njia ya usuluhishi ambayo imesaidia Serikali kupitia Ofisi hii kuokoa fedha nyingi ambazo zitasaidia kuchochea shughuli za maendeleo. Mashauri yaliyoendeshwa kwa njia ya Majadiliano kwa mafanikio nje ya Mahakama ni kama ifuatavyo: -

i) Wallis Trading Inc. dhidi ya Kampuni ya Ndege Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia shauri la madai Na. CL 2017/000227 ambapo majadiliano yalifanyika na kufanikiwa kumaliza shauri hili na hivyo kuwezesha ndege tatu (03) kuachiliwa ambazo zilikuwa zimeshikiliwa nchini Canada;

ii) Lupembe Farmers Joint Co-operative Enterprises dhidi ya Dhow Mecantile Ltd, Lupembe Tea Estate na Msajili wa HAZINA, maombi ya ardhi Na. 582/2022 ambapo Serikali ilikamilisha majadiliano na kufanikiwa kurejesha kiwanda cha Chai Lupembe kwa Serikali na wananchi;

iii) Mnamo tarehe 24/03/2022 katika shauri la Exim Bank Limited dhidi ya Tanzania Fertilizer. Shauri la Biashara Na. 20/2021 Serikali ilifanikiwa kufanya majadiliano kwa deni ililokuwa inadaiwa la zaidi ya dola za Marekani milioni 6 ambapo majadiliano hayo Serikali ililipa dola za Marekani milioni mbili na laki saba tu (2,700,000) na kusadia kuokoa dola za Marekani milioni tatu na laki tatu (3,300,000) ambazo Serikali ingepaswa kuzilipa endapo shauri hili lingeendelea kuendeshwa mahakamani;

iv) Katika shauri la H.H Hilal Co Limited dhidi ya Medical Stores Department & Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Shauri la Madai Na. 105/2015, Ofisi imefanya majadiliano ya kumaliza mgogoro nje ya Mahakama ambayo yalifanikiwa kumshawishi mdai kukubali kulipwa shilingi 1,503,524,720 badala ya shilingi 13,482,774,850 zilizoamriwa kulipwa na Mahakama, hivyo kufanikiwa kuokoa shilingi 11,979,250,130;

v) Kuendesha mashauri ya Kimataifa ambapo mnamo tarehe 29 Juni, 2023 Ofisi kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania ilifanya majadiliano ya Ufilisi wa Benki ya FBME tawi la Tanzania na Cyprus ambapo kwa kumalizika kwa majadiliano kuliwezesha kuteuliwa kwa Mufilisi wa Benki hiyo na kumaliza mvutano uliokuwepo kwa muda mrefu na kuongeza mashirikiano ya kibenki baina ya Benki Kuu Tanzania na Benki Kuu ya Cyprus;

vi) Mafunzo mbalimbali kwa Mawakili. Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendesha mafunzo kwa Mawakili wa Serikali takribani 1,000 kutoka katika Taasisi mbalimbali za Serikali nchini. Mafunzo hayo yaliendeshwa kwa fedha za Serikali mwezi Mei 2021 Arusha na mwezi Mei 2022 Dodoma. Mafunzo hayo yalilenga masuala mbalimbali ya kisheria, uwekezaji, uendeshaji wa mashauri mahakamani, mikataba na hivyo kutengeneza jukwaa la wanasheria wa Serikali kuweza kubadilishana uzoefu na ujuzi.



*Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Balozi Pindi Chana akizungumza na Mawakili wa Serikali wakati akifunga Mkutano wa Chama cha Mawakili wa Serikali uliofanyika kwa siku tatu Jijini Dodoma.*

# Waziri wa Katiba na Sheria asisitiza Mawakili wa Serikali kuwa Waadilifu Wanapotekeleza Majukumu Yao

"Endeleeni kuwa waadilifu na kuwajengea imani wananchi ya kuwaamini watumishi wa umma, nendeni na wazo moja tu la kuwatumikia wananchi kwa weledi, katoeni ushauri wenye tija kisheria kwenye maeneo yenu ya kazi, lazima uwepo wa Wakili au Mwanasheria mahali fulani utambulike."

Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana ametoa wito kwa Mawakili wa Serikali kuzingatia utawala wa sheria na kuendelea kuwa waadilifu katika utekelezaji wa majukumu yao ili kuwajengea imani wananchi wanowatumikia katika utoaji haki.

Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana ameyasema hayo tarehe 22 Machi, 2024 wakati akifunga Mkutano Mkuu wa Chama cha Mawakili wa Serikali wa Tanzania uliofanyika kwa siku tatu katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Jijini Dodoma.

"Endeleeni kuwa waadilifu na kuwajengea imani wananchi ya kuwaamini watumishi wa umma, nendeni na wazo moja tu la kuwatumikia wananchi kwa weledi, katoeni ushauri wenye tija kisheria kwenye maeneo yenu ya kazi, lazima uwepo wa Wakili au Mwanasheria mahali fulani utambulike," alisema Mhe. Balozi Dkt. Chana.

Mhe. Dkt. Pindi Chana amewasihi Mawakili hao wa Serikali kujiendeleza ili kuongeza maarifa akiyataja maeneo ya kipaumbele kuwa ni pamoja na elimu ya uandaaji wa mikataba ya kimataifa, usuluhishi wa mgogoro kwa njia mbadala (Alternative Dispute Resolution - ADR) na matumizi ya akili bandia (Artificial Intelligent) kwa kuzingatia kuwa ulimwengu wa sasa unategemea sana teknolojia kufanikisha masuala mbalimbali.

Kuhusu utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya utoaji wa Msaada wa kisheria ya Mama Samia inayoendelea kutekelezwa kote nchini kwa miaka mitatu tangu ilipozinduliwa Aprili, 2023, amesema Wizara yake inakwenda kuanzisha *kanzi data* ya watoa huduma ya Msaada wa Kisheria ili wajuane na kutambuana katika maeneo yao akiwataka wawe tayari kupokea na kukabiliana na changamoto za wananchi huko walipo, kwani watanzania zaidi ya milioni 61 wanahitaji huduma yao.

Aidha, Mhe. Balozi Pindi Chana alitumia mkutano huo kuipongeza Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kazi wanayoifanya katika kuendelea kusimamia vyema mashauri ya madai na usuluhishi hatua ambayo imesaidia kuokoa fedha nyingi ambazo kama Serikali ingeshindwa basi zingeweza kulipwa na sasa fedha hizo zitasaidia katika kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo kama vile ujenzi wa bwawa la Mwalimu Nyerere, reli ya mwendokasi, miundombinu ya barabara, shule na vituo vya afya nchi nzima.

Akimkaribisha Mgeni Rasmi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Jaji Dkt. Mbuki Feleshi amesema faraja yake ni ustawi wa Mawakili wa Serikali na kuwa yeye ni muumini wa ubora na weledi hivyo ofisi yake itafanya kadri itakavyoweza kuona Mawakili wa Serikali wanakuwa wa viwango vya juu, huku akiwataka kujifunza mambo mengine kutoka kwa wazee akimaanisha yeye mwenyewe na viongozi wengine wa ngazi za juu katika Sekta ya Sheria.

Kwa upande wake Rais wa Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania Wakili wa Serikali Amedeus Shayo amewashukuru Mawakili wote kwa kumchagua kwa kura nyingi na kuahidi kufanya kazi kwa ushirikiano na viongozi wenzake ili kuhakikisha chama hicho kinapiga hatua katika kuyafikia malengo yao kwa muda wote watakaokuwa katika nafasi hizo.

Ameahidi kuweka mpango wa maendeleo ya kitaaluma kwa wanachama kulingana na maendeleo ya teknolojia kwa manufaa ya wanachama wake wote katika nyanja mbalimbali ikiwemo kuendeleza kwa vitendo jitihada za Serikali kuwezesha upatikanaji wa msaada wa huduma za kisheria kwa wananchi kote nchini hasa makundi yenye uhitaji maalumu kwa namna ya kuunga mkono Kampeni ya Mama Samia Legal Aid inayoendeshwa na Wizara ya Katiba na Sheria.

Mawakili wa Serikali walitumia Mkutano huo kumchagua Wakili wa Serikali Amedeus Shayo kuwa Rais wa Chama hicho pamoja na Wakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Rashid Mohamed kuwa Katibu pamoja na viongozi wengine katika nafasi mbalimbali.

Mkutano Mkuu wa Chama cha Mawakili wa Serikali wa Tanzania uliofanyika kwa siku siku tatu, ulianza tarehe 20 hadi 22 Machi, 2024 kwa kufunguliwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb).



*Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi akizungumza na Mawakili wa Serikali wakati akimkaribisha Waziri wa Katiba na Sheria ili aweze kufunga Mkutano wa Chama cha Mawakili wa Serikali uliofanyika kwa siku tatu Jijini Dodoma.*



*Rais wa Chama cha Mawakili wa Serikali wa Tanzania, Wakili wa Serikali Amedeus Shayo akiwashukuru Mawakili wa Serikali kwa kumchagua kwa kishindo kuwa Rais wa Chama hicho katika uchaguzi uliofanyika Jijini Dodoma.*



*Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Pindi Chana akimkabidhi cheti Katibu Mkuu wa Chama cha Mawakili wa Serikali Wakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Rashid Mohamed mara baada ya kutangazwa mshindi wa nafasi hiyo wa chama hicho.*



Dkt. Boniphace Nalija Luhende
Wakili Mkuu wa Serikali

# Migogoro Dhidi ya Serikali Katika Mikataba ya Kimataifa: Nini Kifanyike Ili Wizara na Taasisi Zake Kuepuka Migogoro

"Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekuwa inatoa miongozo ya kuzikumbusha Wizara na Taasisi za Serikali kuzingatia sheria, kanuni na taratibu kabla ya kufikia maamuzi ya kuvunja mikataba ikiwa ni pamoja na kuomba ushauri kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya kuvunja Mkataba"

Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende ametumia Mkutano Mkuu wa Chama cha Mawakili wa Serikali wa Tanzania kuwasilisha mada kuhusu migogoro dhidi ya Serikali katika Mikataba ya Kimataifa na nini kifanyike ili Wizara na taasisi ziweze kuepuka migogoro.

Dkt. Luhende amesema kuwa mada hiyo imelenga kupunguza migogoro inayoweza kujitokeza hasa pale Serikali inapoingia mikataba ya uwekezaji katika sekta mbalimbali ikiwemo miradi mikubwa ya maendeleo ambayo Serikali imekuwa ikitekeleza kwa lengo la kujiletea maendeleo.

Ameongeza kuwa kuongezeka kwa mashauri ya madai na usuluhishi dhidi ya Serikali yanayotokana na madai ya ukiukwaji wa masharti ya mikataba ya kulinda uwekezaji (Bilateral Investment Treaties-BIT) ambapo yapo baadhi ya mashauri ambayo yanaigharimu Serikali kuwalipa wadai kiwango kikubwa cha fedha za kigeni kama fidia.

Dkt. Luhende amezitaja sababu mbalimbali zinazosababisha kuibuka kwa mashauri ambazo ni pamoja na utwaaji wa ardhi au kufuta umiliki wa ardhi bila kufuata taratibu za kisheria, kutolipa fidia kwa wawekezaji, usimamizi usioridhisha wa mradi au uwekezaji unaotekelezwa na kampuni za nje, kuchelewa kutekeleza makubaliano kwa wakati (deed of settlement), amri za mahakama zinazohusu wawekezaji wa nje na uwepo wa taasisi zaidi ya moja za Serikali zinazoshughulikia suala moja lakini mifumo haisomani.

Ameongeza kuwa Serikali imeanza kuchukua hatua kwa kuendesha mashauri kwa njia ya usuluhishi na inashirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuendesha mashauri hayo kwa njia ya usuluhishi.

Amesema utaratibu huo kwa kiasi kikubwa umeokoa muda, gharama kwa Serikali za kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi hatua ambayo imeleta mafanikio katika kupunguza kwa kiwango kikubwa gharama za uendeshaji wa mashauri.

“Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekuwa inatoa miongozo ya kuzikumbusha Wizara na Taasisi za Serikali kuzingatia sheria, kanuni na taratibu kabla ya kufikia maamuzi ya kuvunja mikataba ikiwa ni pamoja na kuomba ushauri kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya kuvunja Mkataba”, alifafanua Dkt. Luhende.

Serikali itaendelea kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali kwa kuwapatia mafunzo endelevu ambayo yatawasiaidia kuendesha mashauri kwa weledi na ufanisi zaidi.

Dkt. Boniphace Luhende ametoa rai kwa viongozi na watumishi wa Serikali kwa pamoja kuzingatia na kuheshimu mikataba ya uwekezaji, sheria, taratibu na kanuni ili kuleta kuleta matokeo chanya katika uendeshaji wa mashauri, mazingira bora ya kuvutia wawekezaji, kupungua kwa gharama na muda wa kuendesha mashauri ya madai yanayofunguliwa nje ya nchi dhidi ya Serikali, kudumisha mahusiano mazuri ya kidiplomasia na kuokoa kiwango kikubwa cha fedha za kigeni zinazolipwa kama fidia na gharama za uendeshaji wa mashauri hayo.




*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa akizungumza na Mawakili wa Serikali wakati akifungua Mkutano wa Chama cha Mawakili wa Serikali wa Tanzania uliofanyika jijini Dodoma.*




*Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakiwa katika picha ya pamoja kwenye banda la maonesho wakati wa mkutano mkuu wa Chama cha Mawakili wa Serikali (PBA) jinini Dodoma.*




*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Usimamizi wa Mashauri na Udhibiti Ubora wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Alice Mtulo kuhusu majukumu ya Ofisi hiyo alipotembelea Banda la Maonesho la Ofisi hiyo kabla ya kufungua Mkutano wa Chama cha Mawakili wa Serikali wa Tanzania uliofanyika jijini Dodoma.*




*Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi akizungumza na Mawakili wa Serikali wakati wa Mkutano wa Chama cha Mawakili wa Serikali wa Tanzania uliofanyika jijini Dodoma.*



*Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Wizara, Taasisi, Mashirika na Halmashauri zote nchini wakifuatilia mada mbalimbali wakati wa Mkutano wa Chama cha Mawakili wa Serikali uliofanyika jijini Dodoma.*

# 4R Katika Kushughulikia Migogoro ya Usuluhishi Dhidi ya Serikali

Idara ya Usuluhishi ni miongoni mwa Idara katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Idara hii ina jukumu la kusimamia, kuendesha na kuratibu kesi zote za usuluhishi ndani na nje ya nchi. Pia, Idara inatoa ushauri wa namna ya kuzuia migogoro pamoja na mafunzo yanayohusu usuluhishi kwa Mawakili wa Serikali na wataalamu kwa ujumla. Idara ina Vitengo viwili ambavyo ni: Mashauri ya Usuluhishi Sehemu ya Ndani ya Nchi (Domestic Arbitration) na Mashauri ya Usuluhishi Sehemu ya Nje Nchi (International Arbitration). Kwa kipindi chote OWMS imeendelea na itaendelea kufanya kazi kwa weledi kuhakikisha kwamba 4R ambazo ni Maridhiano (Reconcilation), Ustahimilivu (Resiliency), Mabadiliko (Reform) na Kujenga Upya (Rebuilding) zinaendelea kutekelezwa kwa vitendo.

Kwa kipindi kwa takribani miaka sita (6) idara imeendelea kuendesha mashauri ndani na nje ya nchi kwa ufanisi mkubwa, kusimamia majadiliano ya mashauri mbalimbali yaliyoko kwenye hatua za usikilizwaji na mashauri yenye tuzo dhidi ya Serikali.

Hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la mashauri ya usuluhishi dhidi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutokana na madai ya ukiukwaji wa masharti ya mikataba baina ya nchi mbili ya kulinda uwekezaji (Bilateral Investment Treaties) hasa kwa wawekezaji kutoka nje ya nchi wanaofanya/waliokuwa wanaendesha shughuli zao hapa nchini kwa nyakati tofauti.

Mashauri hayo yanafunguliwa katika Mahakama ya Kudumu ya Usuluhishi (Permanent Court of Arbitration - PCA), Baraza la Kimataifa la Biashara (International Chamber of Commerce Arbitration Court - ICC), Baraza la Kimataifa la Usuluhishi wa Migogoro ya Uwekezaji (International Centre for Settlement of Investment Disputes - ICSID) na mashauri mengine machache kufunguliwa katika nchi za nje ambako mali za Serikali zinaweza kukamatwa kwa wakati husika pale panapokuwa



Dkt. Boniphace Nalija Luhende
Wakili Mkuu wa Serikali

na tuzo (Arbitral Award) zilizotolewa dhidi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au taasisi zake mfano Canada, Uholanzi, India na Afrika Kusini.

Mashauri haya yanapokwisha, Serikali imekuwa ikiamuliwa kuwalipa wawekezaji/waliokuwa wawekezaji kutokana na kukiukwa kwa Mikataba ya Kulinda Uwekezaji. Mara nyingi tuzo hizo huwa na kiwango kikubwa cha fedha za kigeni zinazodaiwa ambazo iwapo taratibu za ndani ya nchi zingefuatwa malipo yangekuwa ya kiasi kidogo.

Masuala yanayopelekea madai hayo kufunguliwa yanatokana na kukiukwa kwa masharti ya mikataba ya uwekezaji au mikataba ya kibiashara au kushindwa kutekeleza Makubaliano yaliyofikiwa

hasa kumaliza sehemu ya malipo ya Makubaliano ya Kumaliza Mgogoro nje ya Mahakama (Settlement of Deed). Masuala haya ni pamoja na:-

(i) Utwaaji wa ardhi iliyokuwa inamilikiwa na mwekezaji kwa sheria ya Bunge bila kulipa fidia;

(ii) Kufuta hati ya umilki wa ardhi bila kufuata utaratibu wa kisheria au/na kutolipa fidia;

(iii) Kubatilishwa kwa umilki wa ardhi kutoka kwa mwekezaji;

(iv) Taasisi tofauti za Serikali kutoa Leseni za Madini/Mafuta kwa wawekezaji tofauti ndani ya eneo moja;

(v) Madai ya kuongezeka kwa gharama za mikataba (escalation of materials costs);

(vi) Kuvunjwa kwa Mkataba wa kutoa huduma bila kulipa gharama za Mkataba baada ya upande mmoja kutekeleza wajibu wake;

(vii) kukatishwa kwa utekelezaji wa mikataba ya kibiashara;

(viii) Serikali kuchelewa kufanya maamuzi;

(ix) Uwepo wa Taasisi za Serikali zinazoshughulika na suala moja.

Jumla ya mashauri yaliyofunguliwa kwenye mabaraza ya kimataifa ya usuluhishi na mahakama za nje ya nchi kwa kipindi cha miaka mitano 2018-2023 ni arobaini na sita (46). Serikali kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imefanya majadiliano mbalimbali na wadai kwa nia ya kupunguza gharama za madai husika, gharama za uendeshaji wa mashauri hayo katika mabaraza na mahakama za kimataifa na kati ya mashauri hayo, mashauri kumi na sita (16) yalihitimishwa kwa njia ya majadiliano. Majadiliano hayo yalisaidia kupunguza kiasi cha fedha za madai ambacho wadai walilipwa baada ya majadiliano.

Aidha, mashauri yaliyosikilizwa na kuhitimishwa kwenye mabaraza ya kimataifa ya usuluhishi na mahakama za nje ya nchi ni kumi na mbili (12). Vilevile, mashauri nane (8) majadiliano yake bado yanaendelea kwa nia ya kufikia muafaka nje ya mabaraza ya usuluhishi. Pia, kuna mashauri matatu (3) ambayo majadiliano hayakufanikiwa na hivyo yanaendelea kusikilizwa katika mabaraza ya kimataifa ya usuluhishi. Hadi sasa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali zinaendelea kuendesha na kupokea taarifa za nia ya kuishtaki Serikali katika mabaraza ya kimataifa ya usuluhishi ambazo idadi yake mpaka sasa ni kumi na nane (18).

Kwa kipindi cha miaka mitano, Serikali kupitia utaratibu wa majadiliano ya kumaliza mashauri nje ya mifumo ya kimataifa ya kushughulikia migogoro ya uwekezaji na mikataba ya Kimataifa imeokoa kiasi cha dola za Marekani 3, 949, 255,420.35, Shilingi za Tanzania 78,111,197.90 na dola za Canada 176,826.44. Aidha, dola za Marekani 27,902,598.68 kama gharama za uendeshaji wa mashauri zimeokolewa. Mfano wa baadhi ya mashauri na kiasi kilichookolewa kupitia majadiliano ni kama inavyoonekana hapa chini:-

(i) Shauri baina ya Pangea Minerals na Bulyanhulu Gold Mine Limited dhidi ya Serikali (LCIA Arbitration No. UN173686). Katika shauri hili, Kampuni mbili za Madini zilifungua kesi hii kupinga hatua zinazochukuliwa na Serikali ikiwemo kuboresha sheria za usimamizi wa Sekta ya Madini kati ya mwaka 2016-2018 ikiwemo kuzuia usafirishaji wa makinikia. Katika shauri hilo, Serikali ilikuwa inadaiwa takribani dola za Marekani bilioni 3 sawa na shilingi trilioni 7. Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ikishirikiana na Timu maalum ya Majadiliano ya Serikali, tarehe 29 Novemba, 2022 iliweza kumaliza shauri hili kwa majadiliano nje ya usuluhishi. Hivyo, Serikali haikulipa fidia yoyote.

(ii) Shauri baina ya Heritage Rukwa (Tz) Limited dhidi ya Shirika la Maendeleo la Petroli Tanzania (TPDC) na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mdai alikuwa anadai eneo lake alikabidhiwa mwekezaji mwingine kwa ajili ya utafutaji wa madini kinyume na Mkataba wa uwekezaji baina ya Tanzania na Uingereza na hivyo kudai fidia ya kiasi cha dola za Marekani 72,494,138 (sawa shilingi bilioni 170) na pamoja na shilingi 78,111,197.90. Kiasi hicho cha fedha kiliwasilishwa katika Baraza la Kimatifa baada ya majadiliano pande zote zilikubaliana kumaliza mgogoro huu kwa mdai kupatiwa eneo mbadala la uwekezaji. Kwa muktadha huo, Serikali kupitia utaratibu huu wa majadiliano imeokoa kiasi cha dola za Marekani 72,494,138 na shilingi 78,111,197.90;

(iii) Shauri Na. ICSID ARB/17/33 EcoEnergy Africa AB (EcoEnergy) dhidi ya Serikali

ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika Shauri hili, Serikali iliamriwa kuwalipa wawekezaji dola za Marekani milioni 166,971,552 pamoja na gharama ambazo, ikijumuisha na riba hadi kufikia mwezi Aprili, 2023; Serikali ilipaswa kulipa dola za Marekani 175, 891,75. Baada ya majadiliano, pande zote zilikubaliana kushusha madai hayo kuwa dola za Marekani milioni 138.5 hivyo Serikali kupitia utaratibu wa majadiliano umeweza kuokoa dola za Marekani 37.3;

(iv) Shauri baina ya Kampuni ya Winshear Gold Corp. dhidi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (ICSID ARB/20/25). Kampuni ya Winshear Gold Corp ni miongoni mwa makampuni matatu ya madini ambayo yaliwasilisha malalamiko dhidi ya Serikali ya Tanzania katika Baraza la Kimataifa la usuluhishi wa Migogoro (ICSID) ikidai fidia ya dola za Canada 124,781,945.00 kutokana na Serikali kufuta leseni hodhi katika mradi ambao ilikuwa ikiumikili kupitia Kampuni ya Kitanzania ya Bafex Tanzania Limited huko Saza Makongorosi Chunya. Kesi hii ilifunguliwa kwa kuzingatia Makubaliano ya Kulinda na Kuendeleza Uwekezaji na Wawekezaji baina ya Serikali ya Canada na Tanzania. Hata hivyo, Serikali ilifanya majadiliano na Kampuni hiyo na ilikubalika kulipa kiasi cha dola za Marekani million 30 ili kumaliza mgogoro huu.

(v) Shauri Na. ICC 2261/10 Symbion Power Tanzania Limited dhidi ya TANESCO madai ya msingi yalikuwa dola za Marekani 355,563,678.30. Baada ya majadiliano pande zote zilikubaliana kushusha madai hayo kuwa dola za Marekani 153,434,206.83. Kiasi kilichookolewa kupitia majadiliano ni dola za Marekani 202,129,471.47;

(vi) Shauri Na. ICC 15947/VRO Dowans Holding SA (DHSA) na Dowans Tanzania Limited (DTL). dhidi ya TANESCO madai ya msingi yalikuwa dola za Marekani milioni 77.7. Baada ya majadiliano pande zote zilikubaliana kushusha madai hayo kuwa dola za Marekani 52,471,848.77. Kiasi kilichookolewa kupitia majadiliano ni dola za Marekani 25,228,151.83; na

(vii) Mohammed Abdulmohsin Al-Kharafi & Sons for General Trading, General Contracting & Industrial Structures W.L.L (Kuwait) dhidi ya Jamhuri ya Muungano Tanzania; Wizara ya Kazi: na Wakala wa Barabara Tanzania madai ya msingi yalikuwa dola za Marekani milioni thelathini 30,000,000. Baada ya majadiliano pande zote zilikubaliana kushusha madai hayo kuwa dola za Marekani 20,000,000. Kiasi kilichookolewa kupitia majadiliano ni dola za Marekani 10,000,000.

Kama tulivyobainisha kuwa chimbuko la mashauri haya ni ukiukwaji wa masharti ya mikataba ya uwekezaji iliyoingiwa baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nchi mbalimbali. Kwa sasa Tanzania ina mikataba ya uwekezaji na nchi kumi na moja (11) ambayo ipo hai, mikataba nane (8) ambayo sio hai na mikataba miwili (2) ambayo Tanzania imesitisha.

Pia, baadhi ya mashauri yametokana na Serikali au Taasisi zake kutozingatia masharti ya mkataba ya utekelezaji wa miradi ikiwemo masharti ya uvunjaji wa mkataba na mabadiliko ya sheria mbalimbali ambayo yameathiri mikataba iliyoingiwa kabla ya sheria hizo kutungwa hususani Sheria ya Utajiri wa Asili na Maliasili za Nchi (Natural Wealth and Resource (Permanet Soverignty Act of 2017), The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act, 2017 na The Mining (Mineral Rights) Regulations, 2018.

Hatua zilizochukuliwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, chini ya uongozi na usimamizi wa karibu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kukabiliana na mashauri yanayofunguliwa dhidi ya Serikali ni pamoja na kufanya majadiliano ya kusuluhisha migogoro na mashauri yaliyofunguliwa kwenye mabaraza ya kimataifa ya usuluhishi na mahakama za nje. Utaratibu huu unaokoa muda na gharama kwa Serikali. Njia hii imeonyesha mafanikio katika kupunguza kwa kiwango kikubwa kiasi cha madai kabla ya usikilizaji wa mashauri au tuzo baada ya Mabaraza husika kutoa tuzo husika. Hata hivyo, baada ya tuzo kutolewa hali inakuwa ngumu sana katika majadiliano hasa wadai wakijua kuna mali ambayo wanaweza kuikamata.




*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende akimkaribisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi (hayupo pichani) kuzungumza na wajumbe wa Menejimenti wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa mafunzo ya uongozi kwa wajumbe hao yaliyofanyika Kibaha, Pwani.*

# OWMS Yamaliza Mashauri Yenye Maslahi Mapana kwa Taifa

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) imefanikiwa kumaliza mashauri yenye maslahi mapana kwa taifa kwa kusimamia na kuendesha mashauri ya madai, usuluhishi, katiba, haki za binadamu na uchaguzi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake ndani na nje ya nchi ambapo mafanikio hayo yamejikita kwenye mashauri yenye maslahi mapana kwa taifa

Hayo yameelezwa na Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende wakati wa mafunzo ya uongozi na kikao cha faragha kwa wajumbe wa Menejimenti wa Ofisi hiyo wakati akimkaribisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi kuzungumza na wajumbe wa Menejimenti wa Ofisi hiyo leo tarehe 17 Januari, 2024 Kibaha, Pwani

***"Hadi kufikia mwezi Septemba, 2023; OWMS imeendesha jumla ya mashauri 7,393 ya madai na usuluhushi ambapo imefanikiwa kumaliza mashauri yenye maslahi mapana kwa taifa ambayo ni pamoja na shauri la urejeshaji wa ndege ya Serikali nchini; uwekezaji wa kampuni ya DP World; kumaliza shauri la kampuni ya madini ya Winshear kwa njia ya majadiliano ambapo Serikali imelipa dola za marekani milioni 30 badala ya dola za marekani milioni 120 na kuokoa dola za marekani milioni 90; kampuni ya Tanga Cement dhidi ya kampuni ya Twiga Cement; na kumaliza shauri la kuongezewa muda wa utumishi wa Jaji Mkuu," amefafanua Dkt. Luhende***

Ameongeza kuwa wajumbe hao wanapatiwa mafunzo ya uongozi pamoja na mada kuhusu uwekezaji na namna ya kuongeza kipato; mfumo wa mashauri wa Mahakama Kuu; mashauri ya haki za binadamu; maadili ya viongozi; udhibiti ubora; mifumo ya TEHAMA; afya ya akili na saikolojia

Akizungumza kwa wajumbe wa OWMS wakati wa mafunzo hayo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi alisema kuwa OWMS ni Ofisi kubwa na haina mbadala kwa kuwa imebeba dhamana ya nchi.

***"Wanaofanya kazi na OWMS, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka lazima uaminike, tuepuke matatizo yanayoweza kuathiri utendaji kazi wetu na tuzingatie maadili ya utumishi wa umma na miiko ya taaluma zetu," amesisitiza Dkt. Feleshi***

Dkt. Feleshi ametoa rai kwa Mawakili wa Serikali kuzingatia masuala kumi yafuatayo katika utekelezaji wa majukumu ambayo ni kujifunza maarifa na stadi mpya za kazi; kuandaa dondoo za mawasilisho na marejesho wa kazi ulizofanya; kuwa na mawasiliano na mahusiano yenye tija na wenzako au wadau; kutotenda jambo lililo juu ya maelekezo uliyopewa; kuwa mwangalifu katika maneno au mawasiliano unayofanya; kujilinda na uovu na kuwa mwaminifu muda wote kama kuna jambo baya umefanya toa taarifa mapema; kuwa tayari wakati wowote kwa uwakilishi na kutoacha ombwe la uwakilishi pale shauri na Serikali linapotokea halina Wakili husika; kuwajengea uwezo wa kazi wenzako kwa kutekeleza jukumu ulilopewa kwa kuwasaidia, kusimamia na kuwawezesha; na kufanya utafiti bila kukoma

Naye Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Mark Mulwambo alisema kuwa mafunzo ya uongozi yametolewa kwa wajumbe wa OWMS ambapo yanajumuisha ushiriki wa Wakuu wa Idara, wakuu wa Vitengo na Mawakili wa Serikali Wafawidhi wa Mikoa wa OWMS kutoka mikoa 17 ambapo mafunzo hayo yatawawezesha kufanya tathmini ya utekelezaji wa makujumu, kuboresha, na kupanga vipaumbela na malengo ya OWMS kwa mwaka 2024

Imetolewa na:

Prisca J. Ulomi

**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**

17 Januari, 2024




*Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Dkt. Eliezer Feleshi akizungumza na wajumbe wa Menejimenti (hawapo pichani) wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa mafunzo ya uongozi kwa wajumbe hao yaliyofanyika Kibaha, Pwani.*




*Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Mark Mulwambo akizungumza na wajumbe wa Menejimenti (hawapo pichani) wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati akimkaribisha Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende (hayupo pichani) kuzungumza na wajumbe hao wakati wa mafunzo yaliyofanyika Kibaha, Pwani.*



*Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi (aliyeketi katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na wajumbe wa Menejimenti wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa mafunzo ya uongozi yalitolewa kwa wajumbe hao Kibaha, Pwani. Wa pili kulia ni Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende na wa pili kushoto ni Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu Mark Mulwambo.*




*Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi (aliyeketi katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na Mawakili wa Serikali Wafawidhi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa mafunzo ya uongozi kwa Wafawidhi hao yanayofanyika Kibaha, Pwani. Wa pili kulia ni Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende na wa pili kushoto ni Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Mark Mulwambo.*

# HABARI PICHA

Dodoma

## ZIARA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA WALIPOTEMBELEA UJENZI WA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI, MJI WA SERIKALI, MTUMBA JIJINI DODOMA



*Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Mark Mulwambo akimkaribisha Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria na wajumbe wake wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Mji wa Serikali, Mtumba jijini Dodoma.*



*Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ikikagua maendeleo ya ujenzi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwenye Mji wa Serikali, Mtumba jijini Dodoma*



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Bi. Mary Makondo akitoa maelezo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kabla ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Mji wa Serikali, Mtumba jijini Dodoma. Wa kwanza kulia ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mhe. Florent Kyombo.*



*Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Mark Mulwambo akitoa maelezo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kabla Kamati hiyo kuanza kukagua ujenzi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Mji wa Serikali, Mtumba jijini Dodoma.*



*Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Mhe. Yahaya Masare akisisitiza jambo kwa Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Mark Mulwambo (wa kwanza kushoto) wakati wa ziara ya kukagua ujenzi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Mji wa Serikali, Mtumba jijini Dodoma.*



*Picha ya pamoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria; viongozi wa Wizara ya Katiba na Sheria; watendaji wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali; mkandarasi SUMA JKT; na mshauri elekezi TBA baada ya kukagua ujenzi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Mji wa Serikali, Mtumba jijini Dodoma.*

# OWMS Yajiandaa Kupokea Mashauri Ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa



Wakili Mkuu wa Serikali
Dkt. Boniphace Luhende



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende (aliyeketi katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na washiriki wa mafunzo ya uongozi kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yaliyofanyika Kibaha, Pwani.*

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) inajiandaa kupokea mashauri yanayohusu uchaguzi wa Serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika mwaka huu nchi nzima.

Hayo yamesemwa na Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende wakati akifungua mafunzo ya uongozi na kikao cha faragha kwa wajumbe wa Menejimenti wa Ofisi hiyo yanayojumuisha Wakuu wa Idara; Wakuu wa Vitengo; Wakurugenzi Wasaidizi na Mawakili Wafawidhi wa Mikoa 16 wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yanayofanyika kwa siku tano kuanzia leo tarehe 16 Januari, 2024 kwenye ukumbi wa Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Nyerere, Kibaha mkoa wa Pwani.

Dkt. Luhende amewaeleza wajumbe wa Menejimenti kuwa OWMS inasimamia na kuendesha mashauri ya uchaguzi, katiba, haki za binadamu,

madai na usuluhishi hivyo hatuna budi kujiandaa kuendesha mashauri ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa kuwa uchaguzi utafanyika mwaka huu nchi nzima

***"Uongozi ni dhamana, tuna jukumu kubwa la kuiwakilisha nchi ili kulinda rasilimali za taifa na kulinda haki za wananchi kwa maslahi mapana ya taifa hivyo mafunzo ya uongozi ni mkakati wa kufanya tathmini ya utendaji kazi wetu, kuweka dira na mwelekeo wa OWMS ili kuainisha vipaumbele mbali mbali na kuboresha utendaji kazi kwa kuwa Ofisi hii ni muhimu na inategemewa na Serikali kwa maslahi mapana ya Taifa letu," amefafanua Dkt. Luhende.***

Ameongeza kuwa hadi kufikia mwezi Septemba, 2023; OWMS imeendesha jumla ya mashauri 7,393 ya usuluhishi na madai na kuiwezesha Serikali kushinda mashauri hayo ikiwemo kuendesha shauri la ndege ya Serikali na kuweza kuirejesha nchini; imeokoa shilingi bilioni 200 ambazo ni sawa na dola za marekani 90 kwenye shauri la Kampuni ya madini ya Winshear na shauri hilo lilimalizwa kwa njia ya majadiliano ambapo malipo ya dola za marekani 30 yalifanyika badala ya dola za marekani 120; kumaliza shauri la bandari lililohusu kampuni ya DP World; shauri la bomba la mafuta; shauri la kampuni ya Twiga Cement na Tanga Cement; na shauri la nyongeza ya muda wa Jaji Mkuu wa Tanzania.


Amefafanua kuwa mafunzo yatakayotolewa pamoja na masuala ya uongozi ni pamoja na masuala ya uwekezaji wa namna ya kuongeza kipato, utekelezaji wa tuzo za usuluhishi, kupitia mfumo wa mashauri wa Mahakama Kuu, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na mashauri ya haki za binadamu, akili hisia na saikolojia, maadili, miiko na taratibu za uongozi, uibuaji wa miradi ya maendeleo na mapitio ya mpango wa bajeti.

Akizungumza wakati anamkaribisha Dkt. Luhende kufungua mafunzo hayo, Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Mark Mulwambo amesema kuwa madhumuni ya mafunzo hayo ni kujitathmini, kujengeana uwezo baina ya viongozi ili kuweza kusimamia vema watumishi na kufikia malengo yaliyowekwa na kujikumbusha maadili ya viongozi wa umma kwa kuwa sisi wote ni watumishi wa umma

***"Sisi viongozi tunabeba taswira ya Ofisi, tukumbuke mienendo yetu ili kuwa na mtazamo chanya katika utekelezaji wa majukumu," amesema Mulwambo.***

Akizungumza kumwakilisha Mkurugenzi wa Mashtaka, Faraja Nchimbi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ameipongeza OWMS kwa kufanya mafunzo mwanzoni mwa mwaka ili kutathmini utendaji kazi wa mwaka 2023 na kuweka malengo ya mwaka 2024 na kwa kuendeleza ushirikiano baina ya OWMS, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuwa Ofisi hizi tatu ni Ofisi mama za sheria nchini kwa kuwa zinashirikiana katika kuendesha mashauri ya madai, haki za binadamu na mashauri ya kikatiba kwa kuweka msimamo wa pamoja mahakamani katika kuendesha mashauri kwa niaba ya Serikali.

Imetolewa na:



Prisca J. Ulomi

**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**

16 Januari, 2024




*Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu Mark Mulwambo akimkaribisha Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende (hayupo pichani) kufungua mafunzo ya uongozi kwa wajumbe wa Menejimenti na Mawakili Wafawidhi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani.*




*Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Mashtaka, ndugu Faraja Nchimbi akiwasilisha salamu za Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa wajumbe wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa mafunzo ya uongozi kwa wajumbe hao kilichofanyika Kibaha, Pwani.*



*Baadhi ya watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakisikiliza kwa makini mada kuhusu uwekezaji na namna ya kuongeza kipato iliyotolewa na CPA(T), Emilian Busara (hayupo pichani) wakati wa mafunzo ya uongozi yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani.*



*Mkufunzi CPA(T), Emilian Busara akitoa mafunzo ya uongozi kwa baadhi ya watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (hawapo pichani) kuhusu uwekezaji na namna ya kuongeza kipato yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani.*




# OWMS Kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Mashauri wa Mahakama Kuu

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) imeanza kutumia Mfumo wa Mashauri wa Mahakama wa Kieletroniki ili kuongeza uwazi, uwajibikaji, upatikanaji wa taarifa kwa haraka na hivyo kujenga imani kwa wananchi kuhusu utendaji kazi wa vyombo vinavyotoa haki kwa wananchi.

Hayo yameelezwa na Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu Mark Mulwambo wakati akifungua mafunzo elekezi kuhusu Mfumo wa Kieletroniki wa Mashauri ya Mahakama Kuu ya Tanzania (e-CMS) na utunzaji wa nyaraka za Serikali ambapo ufunguzi huo umefanyika mjini Morogoro na kusema kuwa OWMS imeona ni muhimu kwa watumishi wake kupata mafunzo kuhusu Mfumo wa Mahakama wa e-CMS ili waweze kuutumia kwa pamoja na kusomana na mfumo wa usajili wa mashauri wa OWMS (CIMS) kwa lengo la kuboresha utendaji kazi, kuongeza tija na ufanisi katika usajili, matumizi na uendeshaji wa

Mfumo wa Mahakama wa e-CMS unawawezesha wananchi kupata taarifa na kufuatilia mwenendo wa mashauri Mahakamani kwa kupata ujumbe kwenye simu zao za mkononi na barua pepe

mashauri baina ya Mahakama, OWMS, wadau na wananchi.

Ameongeza kuwa Mfumo wa e-CMS umefanikisha yafuatayo ikiwemo utoaji wa taarifa kwa wahusika wa shauri kuwa shauri lao limesajiliwa na kupangiwa Jaji au Hakimu; umetoa mwanya wa kujumuisha taarifa za taasisi nyingine za Serikali ili ziweze kutumika na kusomana; utaendana na taratibu za utendaji wa Mahakama; Majaji wanaandika mwenendo wa mashauri kwenye Mfumo badala ya kuandika kwenye majalada; unapanga mashauri kwa kila Jaji badala ya Jaji mmoja kuwa na mashauri mengi au machache.

Pia, Mfumo wa Mahakama wa e-CMS umefanikisha usajili wa namba ya utambuzi wa kesi ambayo haijirudii na kutumiwa na Mahakama nyingine; umesajili taarifa za mashauri ya Mahakama ya Rufaa ambapo hapo awali haikuwepo; umetambua na kuruhusu matumizi ya taarifa kutoka NIDA, BRELA, Chama cha Mawakili wa Tanganyika, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na taarifa za taasisi nyingine; umetambua na kubaini usajili wa Mawakili na Waendesha Mashtaka halali kwa kuwatambua kwa namba zao na sio vinginevyo.

Ndugu Mulwambo amewapongeza Mahakama Kuu ya Tanzania kwa kujenga Mfumo wa e-CMS kwa kuwa haki itapatikana kwa wakati kwa watu wote bila kujali mahali alipo kwa kutumia TEHAMA na kwa kuzingatia kuwa OWMS ni mdau muhimu. Hivyo, mafunzo kuhusu Mfumo wa e-CMS yalitolewa kwa washiriki 27 kutoka OWMS na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuwawezesha watumishi kubadilishana uzoefu kwenye masuala ya usajili wa mashauri, utunzaji wa kumbukumbu za kielektroniki na namna nzuri ya kuwahudumia wateja wa ndani na nje.

Aidha, amewataka washiriki hao kuzingatia mafunzo hayo ili waweze kutumia ujuzi watakaoupata na kuufanyia kazi kwa uadilifu na usiri katika utendaji kazi kwa kuwa Masjala ya Sheria ni Ofisi nyeti katika kutunza nyaraka za Serikali.

Naye Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Masjala ya Sheria wa OWMS, ndugu Dennice Leonard amesema kuwa Mfumo wa Mahakama wa e-CMS utawawezesha wananchi kupata taarifa na kufuatilia mwenendo wa mashauri Mahakamani kwa kupata ujumbe kwenye simu zao za mkononi na barua pepe.

Pia, Katibu Sheria wa OWMS, Bi. Victoria Kawacha ameishukuru Mahakama ya Tanzania kwa kuanzisha mfumo wa e-CMS kwa kuwa utarahisisha utendaji kazi na kupunguza muda wa kuandika taarifa za mashauri na nyaraka mbali mbali kwenye majalada kwa kuwa taarifa zitapatikana kwenye Mfumo huo.



*Baadhi ya Makatibu Sheria wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali walioshiriki Mafunzo Elekezi kuhusu Matumizi ya Mfumo Mpya wa Mahakama wa Kusajili na Kuratibu Mashauri (e-CMS) wakifuatilia mada kuhusu namna mfumo unavyofanya kazi katika mafunzo yaliyofanyika Mkoani Morogoro.*



# Serikali Mbioni Kuanzisha Kituo cha kushughulikia Kero za Wananchi

Mwanasheria Mkuu wa Serikali
Prof. Jaji Eliezer Mbuki Felishi

> "Umuhimu wa dhana ya haki kwa ustawi wa Taifa: Nafasi ya Mahakama na wadau katika kuboresha mfumo Jumuishi wa Haki Jinai".

Serikali imesema kuwa inaangalia uwezekano wa kuanzisha kituo cha kudumu kitakachokuwa na jukumu la kushughulikia kero za wananchi ili kusaidia kupunguza migogoro kwenye jamii.

Hayo yamesemwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi alipotembelea banda la maonesho la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika maonesho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika katika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma.

Mhe. Jaji Dkt. Feleshi amesema kuwa pamoja na

kuwepo kwa njia mbalimbali za kushughulikia kero za wananchi kama vile Maadhimisho ya Wiki ya Sheria yanayofanyika kila mwaka, Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia inayoendelea kutoa huduma nchini ambapo mpaka sasa imetekelezwa kwenye mikoa sita, tovuti na mitandao ya kijamii bado kuna malalamiko kuhusu migogoro mbalimbali ambapo kuanzishwa kwa kituo hiki kutasaidia kumaliza na kutatua kero mbalimbali kwenye jamii zetu zinazotuzunguka.

Aliongeza kuwa kutokana na njia zinazotumika kwa ajili ya kushughulikia malalamiko ya wananchi tungeweza kusema sasa mifumo ya kupokelea maoni na malalamiko inatosha, lakini unaona malalamiko bado yapo, bado wananchi wana kero, mfano migogoro ya ardhi na mirathi.

Alieleza kuwa Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wadau wengine wanaohusika na masuala ya kisheria inaangalia uwezekano wa kuanzisha kituo cha kudumu kama njia ya nyongeza ya kutoa huduma za kisheria kwa maana ya kuelimisha umma kuhusu masuala ya sheria ili kupokea malalamiko na kutoa huduma za kisheria.

“Pamoja na maadhimisho ya Wiki ya Sheria yanayofanywa na Mahakama kila mwaka, Serikali imejitahidi kutumia njia tofauti za kuwafikia wananchi katika kuelimisha na kushughulikia masuala mbalimbali ya kisheria ikiwemo njia za TEHAMA kupitia tovuti, Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, vipindi vya TV na redio, lakini bado kuna malalamiko, hivyo ni muhimu kuwa na kituo cha kudumu ambacho kitakuwa kinatoa huduma kwa wananchi wakati wote,” amesema Mhe. Dkt. Feleshi.

Katika hatua nyingine Mhe. Jaji Dkt. Feleshi ameipongeza Mahakama ya Tanzania, waratibu na waandaji wa Maadhimisho ya Wiki ya Sheria kwa kutenga banda maalumu liliowakutanisha wadau wa Haki Jinai hatua ambayo imesaidia kutatua kero mbalimbali za wananchi na kwa muda mfupi.

Maadhimisho haya ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika katika viwanja vya Nyerere Square yalizinduliwa tarehe 27 Januari, 2024 na kuhitimishwa tarehe 1 Februari, 2024 yakiwa yamebeba kauli mbiu isemayo, *"Umuhimu wa dhana ya haki kwa ustawi wa Taifa: Nafasi ya Mahakama na wadau katika kuboresha mfumo Jumuishi wa Haki Jinai"*.




*Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakitoa elimu ya msaada wa kisheria kwa wananchi waliotembelea Banda la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika Jijini Dodoma.*



*Wakili wa Serikali Mfawidhi Mkoa wa Dodoma wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Janipher Kaaya akitoa elimu ya Msaada wa Sheria kwa wanafunzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika Jijini Dodoma.*

# Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu Watakiwa Kufahamu Sheria za Vyuo Vyao

Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu nchini wametakiwa kuhakikisha wanafahamu sheria, kanuni na miongozo mbalimba ya vyuo ili waweze kujua taratibu za kufuata ili kupata haki zao pindi wanapokutwa na changamoto za kitaaluma.

Wito huo umetolewa na Wakili wa Serikali Mfawidhi wa Mkoa wa Dodoma Bi. Janipher Kaaya, wakati akitoa elimu ya msaada wa kisheria kwa wanafunzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara Kampasi ya Dodoma (CBE) wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika jijini Dodoma.

Ameeleza kuwa kufahamu sheria, kanuni na miongozo hiyo kutawasaidia wanafunzi hao, kufahamu kwa kina kuhusu haki na wajibu wao wakati wa mitihani, kama wanafunzi ili ziweze kuwasaidia kutimiza wajibu wa kuzingatia kanuni za uadilifu wanapokuwa vyuoni.

Kaaya aliongeza kuwa, kufahamu sheria na taratibu kunaweza kuwasaidia wanafunzi hao kuepuka ukiukwaji wa sheria za mitihani kama vile vitendo vya udanganyifu wakati wa mitihani ikiwemo kuvunja kanuni nyingine za chuo ambazo zinaweza kuwa na matokeo mabaya kama vile kusimamishwa masomo pamoja na kufukuzwa chuo.

Alifafanunua kuwa Kupitia Sheria za chuo wanafunzi hao wataweza kufahamu miongozo kuhusu muda wa mitihani, ratiba, na utaratibu wa kupata matokeo hatua itakayosaidia kujua na kufuata taratibu, hatua itakayowasadia kujiandaa vizuri na kuepuka matatizo yanayoweza kutokea kabla,wakati na hata baada ya mitihani.

Alisema kuwa kujua sheria hizo vizuri kutawasaidia wanafunzi hao kujua jinsi ya kutoa malalamiko pamoja na taratibu za kufuata wakati wa kukata rufaa kulingana na sheria za chuo pale wanapokumbwa na matatizo au malalamiko kuhusu mitihani ikiwa hawakuridhika na maamuzi ya awali.

Bi. Kaaya alisisitiza kuwa kufuata sheria na taratibu wakiwa chuoni kutawasaidia wanafunzi kuepuka adhabu au vikwazo vinavyoweza kutokana na ukiukwaji wa sheria za chuo hasa udanyanyifu wakati wa mitihani ikiwa ni pamoja na kuweza kufuata njia sahihi zinazokubalika wakati wa kudai haki zao.

Alisema kuwa kufahamu na kufuata sheria za chuo kikamilifu kutawasaidia wanafunzi wa vyuo mbalimbali nchini kuelewa haki na wajibu wa mwanafunzi ambayo inajumuisha haki za kupata elimu bora, vifaa vya kujifunzia, pamoja na kuongeza uelewa kuhusu wajibu wa kutoa heshima kwa wanafunzi wenzao, wananchi na wafanyakazi wa chuo.

Sheria hizi pia zitasaidia kujenga wanafunzi wenye maadili na tabia njema wakiwa vyuoni hatua itakayosaidia kujenga kizazi bora chenye maadili hata baada ya kumaliza chuo ili waweze kuishi vizuri kwa heshima na ushirikiano na jamii inayowazunguka.

Kufahamu sheria na kanuni za chuo kutawasaidia kufahamu taratibu na miongozo ya kitaaluma pindi wanapohitaji kuchagua au kuhama kozi ili waweze kusoma kozi zenye soko na hatimae iweze kuwasaidia kuhitimu masomo yao kwa ufaulu wa juu.

*Wanafunzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) wakimsikiliza Wakili wa Serikali Mfawidhi Bi. Jenifer Kaaya wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (hayupo pichani) wakati akitoa Elimu ya Msaada wa Kisheria wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika Jijini Dodoma.*





*Wakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu Charles Mtae akitoa elimu ya Msaada wa Sheria kwa wanafunzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika Jijini Dodoma.*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

Simu: +255 22 2127384
Nukushi: +255 22 2127384
Tovuti: www.osg.go.tz
Barua Pepe: info@osg.go.tz

S.L.P 71554
10 Barabara ya Kivukoni
11405 Dar es Salaam
TANZANIA

**09 Machi, 2024**

## *SERIKALI YASHINDA SHAURI LA USULUHISHI KATIKA BARAZA LA KIMATAIFA LA BIASHARA (ICC)*

Tarehe 06 Machi, 2024, Baraza la Kimataifa la Biashara (International Chamber of Commerce-ICC) limetoa uamuzi wake na *kuipa Serikali ushindi* katika Shauri la Usuluhishi Na. 2682/AZO baina ya Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (Petroleum Bulk Procurement Agency-PBPA) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali *dhidi* ya Kampuni ya Alchemist Energy Trading DMCC kutoka Umoja wa Falme za Kiarabu.

Shauri hili lilifunguliwa baada ya Kampuni ya Alchemist Energy Trading DMCC kushindwa kusambaza mafuta kwa mujibu wa Mkataba ulitokana na Zabuni Na. PBPA/CPP/PMC/C3-KOJI/02/2021 wa tarehe 05 Januari 2021 kwa ajili ya kuleta nchini mafuta Metriki za Ujazo 36,192 ambayo yalipaswa kupokelewa kuanzia tarehe 27 Februari, 2021 hadi tarehe 01 Machi, 2021.

Kwa upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ***jopo la utetezi liliongozwa na Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende*** akishirikiana na Mawakili wengine kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA).

Katika uamuzi wake, Baraza la ICC limetamka kuwa Kampuni ya Alchemist Energy Trading DMCC ilivunja Mkataba na hivyo kuwaamuru ***kurejesha fedha kwa Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA) dola za Marekani milioni tisa, laki saba na kumi elfu, mia sita hamsini na moja na senti arobaini na tano (USD 9,710,651.45) pamoja na riba kabla ya tuzo (pre-award interest) asilimia 7.67% kuanzia tarehe 18 Mei, 2021 hadi Novemba, 2023; kwa kuvunja Mkataba na kushindwa kuleta mafuta nchini.***

Pamoja na Kampuni ya Alchemist Energy Trading DMCC kuamuriwa na Baraza hilo kurejesha fedha tajwa hapo juu kwa kuvunja Mkataba, pia Kampuni hiyo inatakiwa kutekeleza yafuatayo:-

***(i) Kuilipa PBPA dola za Marekani milioni moja, laki moja arobaini elfu, na arobaini na nane (USD 1,140,048.00) ikiwa ni adhabu ya kuharibu mfumo wa ununuzi wa mafuta wa pamoja;***

***(ii) Kuilipa PBPA dola za Marekani laki nane themanini na mbili elfu (USD 882,000.00) ikiwa ni gharama za Baraza;***

***(iii) Kuilipa PBPA shilingi milioni mia nane kumi na nane elfu, laki mbili themanini na tano na mia saba (TZS 818,285,700.00) ikiwa ni gharama za kesi; na***

(iv) ***Kulipa riba baada ya tuzo (post award interest) asilimia 7.67% kuanzia tarehe 06 Machi, 2024 hadi atakapokamilisha malipo yote anayodaiwa.***

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inatoa shukrani za dhati kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, PBPA na wadau wote walioshiriki katika kuendesha shauri hili la kimataifa kwa kutumia Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali itaendelea kusimamia na kuendesha mashauri ya kimataifa kwa weledi na kulinda maslahi mapana ya Taifa letu.

Imetolewa na:

Prisca J. Ulomi

**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**



# PEPMIS kuongeza uwajibikaji kwa Watumishi wa Umma

Mwanzo Serikali ilikuwa ikitumia mfumo wa wazi wa mapitio na upimaji wa utendaji kazi (OPRAS) kusimamia utendaji kazi wa watumishi wa umma lakini kutokana na changamoto zake Serikali ilifanya maboresho na kuanzisha mfumo mpya ili kuongeza tija na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu kwa maendeleo ya Taifa.

Serikali imedhamiria kuimarisha utumishi wa umma kwa kuongeza uwajibikaji wa hiari kwa watumishi kwa kujaza majukumu wanayotekeleza kila siku kupitia mfumo wa PEPMIS na PIPMIS mahali popote ili kuongeza tija katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Hayo yameelezwa na Afisa Utumishi Mkuu kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Ramadhani Kauzeni, wakati wa kufungua mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa Kupima Utendaji Kazi wa Watumishi wa Umma na Taasisi (PEPMIS na PIPMIS) na kwa viongozi na watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Ndugu Kauzeni ameeleza kuwa mfumo wa PEPMIS utawawezesha viongozi kusimamia utendaji kazi wa watumishi wanaowasimamia bila upendeleo huku ukiongeza ufanisi, wakati kwa

upande wa mfumo wa PIPMIS utaiwezesha kupima utendaji kazi wa taasisi za umma ili kuhakikisha taasisi zinatekeleza majukumu yake kwa wakati.

Mkufunzi huyo aliongeza kuwa mfumo wa PEPMIS umekuja wakati sahihi kwa kuwa unachukua nafasi ya mfumo wa awali uliotumika kupima utendaji kazi kwa watumishi wa Umma ambao ni OPRAS ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alilolitoa kwenye Sherehe za Mei Mosi mwaka 2023, akisisitiza kuimarisha mifumo ya uwajibikaji inayowezesha viongozi na watumishi wa umma kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Naye Afisa Utumishi Mkuu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na mratibu wa mafunzo hayo Lawrence Mhelela, ameishukuru Serikali kwa kuanzisha mfumo huo kwa kuwa utawawezesha kutekeleza majukumu yao kwa wakati.



*Mchumi wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Ndg. Rashid Shedefa (aliyesimama katikati) akitoa mafunzo kuhusu Mfumo wa PEPMIS na PIPMIS kwa Kaimu Mkurugenzi Idara ya Mipango, Jumanne Gwau na Mchumi, Bi. Zuhura Kussaga wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.*



*Mkurugenzi Msaidizi Usuluhishi wa Kimataifa wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Salome Magesa akipatiwa mafunzo kutoka kwa wataalamu wa mfumo wa PEPMIS na PIPMIS kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Rashid Shedefa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Nyamhoni Chacha (wa kwanza kulia) yaliyofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI



# TANZIA

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inasikitika kutangaza kifo cha aliyekuwa Wakili wa Serikali Mwandamizi ndugu **Solomon Lukombeso Lwenge** kilichotokea tarehe 20 Februari, 2024 alipokuwa akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufaa ya Shinyanga.

**1969 - 2024**

**Bwana Alitoa, Bwana ametwaa, Jina lake Lihimidiwe.**



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende akisaini kitabu cha maombolezo nyumbani kwa aliyekuwa Wakili wa Serikali Mfawidhi mkoani Shinyanga marehemu Solomoni Lwenge, Wangingo'ombe mkoani Njombe.*



*Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu Mark Mulwambo akizungumzia safari ya utumishi wa umma ya aliyekuwa Wakili wa Serikali Mfawidhi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Shinyanga marehemu Solomoni Lwenge wakati wa ibada ya mazishi yake yaliyofanyika nyumbani kwao Wanging'ombe mkoani Njombe.*



*Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu James Kibamba akisoma wasifu wa aliyekuwa Wakili wa Serikali Mfawidhi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Shinyanga marehemu Solomoni Lwenge wakati wa ibada ya mazishi ya mfawidhi huyo yaliyofanyika nyumbani kwake Wanging'ombe mkoani Njombe.*




*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Kuhende (kushoto) na Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu Mark Mulwambo wakiweka shahada la maua kwenye kaburi la aliyekuwa Wakili wa Serikali Mfawidhi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Shinyanga marehemu Solomoni Lwenge wakati wa ibada ya mazishi yaliyofanyika nyumbani kwake Wanging'ombe mkoani Njombe.*

JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA
**OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI**

**OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI**
**10 Barabara ya Kivukoni**
**S. L. P 71554**
**11101 DAR ES SALAAM**

**Simu: +255 22 2127384**
**Fax: +255 22 2127385**
**Nukushi: www.osg.go.tz**
**Barua pepe: info@osg.go.tz**

## ANUANI ZA POSTA NA MAENEO ZILIPO OFISI ZA WAKILI MKUU WA SERIKALI MIKOANI

| | |
|---|---|
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 1902<br>41218 DODOMA<br>Jengo la Katiba na Sheria (UDOM)<br>Barua pepe: dodoma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 130<br>31101 MUSOMA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: mara@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 1280<br>63114 MTWARA<br>Maadili House<br>Barua pepe: mtwara@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 394<br>33101 MWANZA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: mwanza@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 595<br>51108 IRINGA<br>Lilokuwa jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Iringa<br>Barua pepe: iringa@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 106<br>35102 BUKOBA<br>Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Mhakiki Mali<br>Barua pepe: kagera@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 564<br>57101 SONGEA<br>Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: ruvuma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 43<br>37101 SHINYANGA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: shinyanga@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 60<br>21101 TANGA<br>Jengo la Mkonge<br>Barua pepe: tanga@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 119<br>45112 TABORA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: tabora@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 202<br>25101 MOSHI<br>Jengo la TRA Moshi<br>Barua pepe: kilimanjaro@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 690<br>55103 SUMBAWANGA, Mtaa wa Ukaguzi<br>Jengo la Ukaguzi, Gorofa ya pili<br>Barua pepe: rukwa@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 66<br>23101 ARUSHA<br>Jengo la AICC, Arusha<br>Barua pepe: arusha@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 710<br>53107 MBEYA<br>Jengo la Madini<br>Barua pepe: mbeya@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 172<br>47101 KIGOMA, Jengo la NHC, Ghorofa ya Pili,<br>Kiwanja Na. 148 & 149, Mtaa wa Lumumba.<br>Barua pepe: kigoma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>Jengo la NSSF, Ghorofa la Nne<br>MOROGORO, Barabara ya zamani DSM<br>Barua pepe: morogoro@osg.go.tz |